

**JIMBO KATOLIKI LA MOROGORO
SHULE YA SEKONDARI ALFAGEMS (S. 3874)**

S.L.P. 6083 – Morogoro

Simu: 0689-783630 (Ofisi Taaluma) / 0789-978886 (Airtel Money)
0689-783672 (Bweni la kike) / 0689-782670 (Bweni la kiume)
www.alfashule.ac.tz

TARATIBU ZA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA

Ndugu tunafurahi kukujuishwa
umepata nafasi ya kujiunga na kidato cha kwanza kwenye shule yetu iliyoko katika manispaa ya Morogoro,
kata ya Tungi, mtaa wa Mji Mwema (kati ya Msamvu na Nanenane). Karibu sana!

Hakuna malipo zaidi ya ada ambayo ni:

- (a) Kwa mwanafunzi wa kutwa Tsh. 500,000 kwa mwaka.
- (b) Kwa mwanafunzi wa bweni Tsh. 1,000,000 kwa mwaka.

Unaruhusiwa kulipa kwa mikupuo minne, yaani Tsh. 125,000, au 250,000 kabla ya kila nusu muhula,
lakini bila robo hiyo hutapokewa.

Kwa usalama wa wote unaombwa ulipie benki (akaunti yenye jina la shule iko MKOMBOZI C.B. ikiwa na
namba 00120603517801; iko pia CRDB, namba 01J2077746000) halafu vocha uilete shulenii katika ofisi ya
mhasibu upate risiti. Nje ya hapo usitoe pesa kwa yeyote, hata kwa walimu wetu: malipo ya namna hiyo si
halali, hivyo shule haihusiki nayo. Jihadhari sana!

Shule imekubaliwa pia kuwa wakala wa kampuni za simu kwa ajili ya kutuma pesa kwa urahisi zaidi.

Namba ya Airtel Money ni 0789-978886 na inatumika kwa mawasiliano na kwa kutuma pesa.

Masomo yataanza tarehe 7-1-2020. Basi:

(a) Ukitaka kuwa mwanafunzi wa kutwa ufile shulenii tarehe hiyo saa 1:15 asubuhi. Ukichelewa wiki moja
kuripoti na kuleta vocha ya benki nafasi yako anaweza akapewa mwininge.

(b) Ukitaka kukaa bweni ufile kabla ya saa 10:00 jioni ya tarehe iliyotangulia mwanzo wa masomo (kwa
kuwa nafasi hazitoshi kwa wote, watapewa waliovahili kuleta ofisini mwetu vocha ya benki hata kabla ya
tarehe hiyo).

Ukichelewa wiki moja kujisajili kwa malipo, nafasi yako atapewa mtu wa akiba.

Ulete kivuli cha cheti cha kumaliza darasa la saba na vitu vilivyoordodheshwa hapa chini:

1. Sare kama ifuatavyo (huruhusiwi kuleta nguo za aina nyingine):

- (a) Kwa wasichana:
 - (i) Shati jeupe lenye maandishi ya shule
 - (ii) Sketi ya rangi ya damu ya mzee (ifikie
sentimeta 25 kutoka ardhini)
 - (iii) Viatu vyeusi visivyo na visigino virefu
 - (iv) Soksi nyeupe zisizo na urembo wowote
 - (v) Sweta ya rangi ya damu ya mzee
 - (vi) Kwa michezo: fulana yenye maandishi ya
shule, trakisuti na raba
 - (vii) Masista wanaruhusiwa kuvaa sare ya
shirika
 - (viii) Waislamu, kwa ombi la mzazi/mlezi,
wanawenza wakaruhusiwa kuvaa hijabu halisi
nyeuepe isiyo na mapambo mradi wanyoe
nywele zote

- (b) Kwa wavulana:
 - (i) Shati jeupe lenye maandishi ya shule
 - (ii) Suruali ya rangi ya damu ya mzee
 - (iii) Viatu vyeusi visivyo na visigino virefu
 - (iv) Soksi nyeupe zisizo na urembo wowote
 - (v) Sweta ya rangi ya damu ya mzee
 - (vi) Kwa michezo: fulana yenye maandishi ya
shule, bukta ya buluu na raba
 - (vii) Mabradha wanaruhusiwa kuvaa sare ya
shirika.

2. Kwa kukaa bweni:

- (a) Fulana ya kijani yenye maandishi ya shule
- (b) Nguo ya kulalia na ya kwenda bafuni
- (c) Mashuka na blanketi
- (d) Chandarua kilichotiwa dawa
- (e) Godoro la futi mbili unusu
- (f) Ndoo
- (g) Sanduku imara na salama
- (h) Tauilo na vifaa vingine vya usafi
- (i) Sahani, bakuli, kikombe na kijiko
- (j) Nauli ya kurudi nyumbani wakati wowote.

N.B. Ni lazima mashati na fulana za shule, sketi, suruali na sweta vinunuliwe shulenii.

Magodoro, mashuka, vyandarua, ndoo, madaftari, kalamu na vifaa vya hisabati pia vinapatikana kwa bei
nafuu.

